DAWASA
Dar es Salaam Water Supply & Sanitation Authority
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

# OFA MAALUM YA KURUDISHIWA HUDUMA YA MAJI BILA KULIPA FAINI

**9.05.2025**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) inapenda kuwajulisha Wananchi na wateja wake kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan** kupitia Wizara ya Maji imetoa ofa maalum kuondoa faini ya kurejeshewa huduma (**reconnection fee**) kwa Wateja wanaodaiwa na Mamlaka za Maji Nchini.

**DAWASA** inawataarifu Wateja wake waliositishiwa huduma sababu ya madeni ya bili za maji kufika katika ofisi za Mamlaka zinazowahudumia ili kuingia mkataba wa kulipa madeni yao na kurejeshewa huduma bila faini ya **Shilingi 15,000**.

Wahi sasa unufaike na ofa hii maalum ambayo imeanza tarehe **9.5.2025** hadi **31.5.2025**

Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja **0800110064** (Bila malipo) au **0735202121** (Whatsapp tu)

Imetolewa na

**Kitengo cha Mawasiliano**